Twitter Thread by Charles John



Charles John
@Gibu_Jr

Tupate Madini 🙏🙏■

Tambua Namna ya kujua kama mileage ya Gari unayotaka kununua Yard au kwa mtu ni sahihi au imechezewa..kurudishwa nyuma■■



TBS walitoa nakala ya kampuni ambayo magari yote yanayokuja Tanzania kutokea Japan wanatumia EAA COMPANY LTD.ambapo hawa kazi zao ni kufanya ukaguzi ambayo gari ikikidhi vigezo wanatoa certificate ya Roadworthness ,pia hawa wanakuwa na E-certificate mtandaoni ambapo huwa mbili

Exporter na nyingine General Public/client E-certificate
Hiyo maada ni ndefu twende kwenye hoja
INSPECTION MILEAGE. ni hapa tunakagua gari tangu imetoka Japan mpaka imefika Tanzania imetumia miezi Michache Mfano
Kuna gari niliiona chases number nikaingia kujua

Imeingia TZ miezi michache kwa kuwa kwenye mwezi wa 9 ilifanyiwa inspection plus shipping days na gari inatembelea chases number odd inasoma 54120 lakini nilivyoingiza chases kwenye website ya EAA inspection mileage kule Japan Km 155,200 kwa maana km zimechezewa Teyari

Kutaka ku verified hatua hizi
1- Tafuta chases number ya gari unayotaka kununua
2-ingiza kwenye website EAA(E-certificate
3-mara nyingi zinakuwa kwenye mfumo wa xxxx-xxx
4-kisha check details utaona taarifa za gari ikiwepo inspected mileage
Tuishi humo.